## Maswali

1. Mbona wachungaji wa Abramu na wachungaji wa Lutu waligombana?
2. Abramu na Lutu waliamua wafanye nini?
3. Abramu alifanya nini kuonyesha alikuwa mzuri na mkarimu?
4. Lutu alichagua aishi wapi?
5. Mbona Abramu alifurahia pahali alipachagua?
6. Nani alipendezwa na Abramu?
7. Mungu alimwambia Abramu afanye nini?
8. Ahadi gani mpya yenye Mungu alimpa Abramu?
9. Mungu aliahidi nini kuhusu uzao wa Abramu?
10. Abramu atapata lini nchi aliyoahidiwa na Mungu?

## Majibu

1. Hakukuwa nyasi na maji ya kutosha mifugo yao yote.
2. Waliamua kutengana.
3. Abramu aliacha Lutu achague kwanza.
4. Lutu alichagua bonde la Yordani.
5 Abramu hakutaka kuwa rafiki wa watu waovu. Aliamini kwamba Mungu atamlinda.
6. Mungu
7. Mungu alimwambia Abramu aangalie pande zote za nchi.
8. Mungu aliahidi kumpa Abramu nchi yote milele.
9. Mungu aliahidi Abramu kwamba atakuwa na wazao wengi wenye hawatahesabika. Kama mchanga wa pwani.
10. Wakati Yesu atarudi kusimamisha Ufalme wa Mungu hapa duniani.

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

## Awamu ya 2    Mwaka wa 1

# 5 Abramu na Lutu

**Kwa Biblia** Mwanzo 13

### Kiini cha somo

Kuonyesha vile Abramu na Lutu walitengana. Abramu alikuwa mzuri na mkarimu. Aliamini Mungu na Mungu alimwambia ahadi zingine nyingi.

### Somo

Abramu, Sarai na Lutu waliishi nchi ya Kanaani kwenye walipelekwa na Mungu. Watu wa Kanaani walikuwa wa nguvu na wakali. Abramu na Lutu walikaa pamoja na watumishi wao waliolinda mifugo yao. Mungu aliwabariki.

Mifugo kama kondoo na mbuzi walikuwa wanyama wa maana sana. Ili mtu aitwe tajiri lazima awe nao wengi. Kutoka kwa mbuzi walipata maziwa, nyama na ngozi, hata ya kutengenezea mahema za kuishi. Kondoo waliwapa nyama na sufu ya kutengeneza nguo. Nchi ya Kanaani ilikuwa kavu na ya joto. Wakati wa kiangazi, nyasi na mito nyingi zilikauka. Abramu na Lutu waliishi kwenye mahema ili iwe rahisi kuhama na mifugo yao wakitafuta nyasi.



Baada ya mda Abramu na Lutu walitajirika sana. Walikuwa na n'gombe na mifugo wengine wengi. Kwa ajili ya hawa mifugo wengi, nyasi na maji haikuwatosha.

Hali ilikuwa mbaya. Wachungaji wa Abramu na Lutu walianza kubishana na kupigania nyasi na maji.

Vita viliendelea na vikawa vibaya sana. Mwishowe Abramu na Lutu waliamua kwamba ni vyema watengane. Waliamua waende kila mtu upande wake kujitafutia nyasi mzuri na wachimbe visima vya maji.

Abramu alikuwa wa umri kuliko Lutu. Angepewa nafasi ya kuchagua upande gani wa kuenda kabla ya Lutu. Lakini Abramu alikuwa mtu mzuri na mkarimu. Alimpa Lutu nafasi achague kwanza.

Abramu na Lutu walienda juu ya kilima. Juu ya hicho kilima wangeona nchi yote mpaka mbali.

Lutu aliangalia na akaona mpaka Mto wa Yordani. Mto uliwezesha nyasi kuwa nyepesi na ya manjano. Kulikuwa na maji mengi kwa huo mto. Kulikuwa na bonde iliyokuwa na miji mingi na huko Lutu angekuwa na marafiki.

Halafu Lutu akaangalia upande mwingine. Hakukuwa na mto. Itakuwa kazi ngumu kuchimba visima vya maji. Vilima havikukuwa na nyasi nyingi. N'gambo ya vilima kulikuwa na jangwa. Jangwani mimea haikui sana.

Lutu alichagua bonde la Yordani. Aliambia Abramu, "Kwa heri." Akaenda kwa bonde la Yordani. Lutu alifurahi kwa sababu alikuwa amechagua mahali pazuri pa kuishi. Alikuwa na maji mengi na nyasi ya mifugo yake. Kulikuwa na miji na akapata marafiki huko.

Abramu alifurahia nchi aliyobaki nayo. Alijua kwamba watu wa bonde la Yordani walikuwa waovu sana. Abramu hakutaka kuwa rafiki wa watu waovu. Abramu alikuwa rafiki wa Mungu. Abramu hakujali kazi ngumu ya kuudumia mifugo yake. Hakujali kwamba hakukuwa na nyasi nyingi. Alijua Mungu atamshugulikia.

Abramu alisimama juu ya kilima. Alikuwa akipanga vile atapata nyasi na kuchimba visima vya maji. Mungu akanena na Abramu. Mungu alipendezwa kwa vile Abramu alikuwa mkarimu na mzuri. Mungu alipendezwa kwa vile Abramu hakutaka kuwa rafiki wa watu waovu. Mungu alipendezwa kwa vile Abramu alimwamini. Mungu aliahidi Abramu ahadi ingine.

Huko juu kwa kilima, Mungu alimwambia Abramu aangalie. Aangalie pande zote mpaka upeo wa macho yake. Mungu alimwaahidi kwamba atampa hiyo nchi **YOTE** pamoja na bonde nzuri la Yordani. Mungu atampa Abramu nchi ya Kanaani yote hata **MILELE.**

Mungu alimwambia Abramu ateremke chini ya kilima. Alimwambia asafiri katika nchi yote akiingalia. Mungu atampa nchi hiyo yote.

Mungu alirudia ahadi zenye alikuwa amemwambia Abramu hapo awali. Alimwaahidi kwamba atakuwa na uzao mkubwa wenye hauwezi kuhesabika. Mungu alimwambia, "Hauwezi kuhesabu mchanga ya pwani, vile vile hautaweza kuhesabu uzao wako, kwa sababu watakuwa wengi mno."

Abramu aliishi nchi ya Kanaani mpaka mwisho wa maisha yake. Lakini hakupewa pahali hata padogo. Abramu hakupewa pahali popote pakuweka hata mguu moja! Sarai mkewe alipokufa hakukuwa na mahali pakumzika. Ilimlazimu anunue sehemu ndogo la shamba ili amzike.

Yaani Mungu alisahau ahadi zake kwa Abramu?

Hapana. Mungu huwa anatimiza ahadi zake. Hivi karibuni Yesu atarudi hapa duniani. Yesu atafufua Abramu kutoka kwa wafu. Hapo ndio Abramu atapewa nchi. Abramu ataishi katika Ufalme wa Mungu milele. Abramu atapewa nchi wakati Yesu atarudi kusimamisha Ufalme wa Mungu hapa duniani.